

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA SITA

23 APRILI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA SITA – TAREHE 23 APRILI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS
(MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

III. MASWALI:

WAZIRI MKUU:

**129. MHESHIMIWA AMINA DAUD HASSAN (VITI
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni lini Serikali itaondoa tatizo la ucheleweshaji wa malipo ya mafao kwa Wastaafu Wanachama wa NSSF.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

130. MHESHIMIWA MAIMUNA SALUM MTANDA (NEWALA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

- 
- The emblem of the Republic of Tanzania is centered in the background. It features a shield with a map of the country, flanked by two figures holding a torch and a staff. A banner at the bottom bears the national motto "UHURU KUUZA UMOJA WA TAIFA".
- (a) Je, ni lini Serikali itaongeza bajeti ya barabara za Newala Vijijini ambayo imetengewa fedha za Km 340 wakati mtandao wa barabara ni Km 960;
 - (b) Je, Serikali inatoa msaada gani wa dharura kwenye matengenezo ya barabara za Vijiji vinavyozungukwa na milima au mito kama vile Mkongi-Nanganga, Mikumbi-Mpanyani, Namdimba-Chiwata, Mkoma-Chimenena na Miyuyu – Ndanda.

131. MHESHIMIWA LIVINGSTONE KABOYOKA NAGHENJWA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka vitendea kazi katika Kituo cha Afya Kata ya Mtii Jimbo la Same Mashariki baada ya kukamilika kwa vyumba 12 vya Jengo la OPD.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**132. MHESHIMIWA ZUENA ATHUMANI
BUSHIRI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, ni lini Jengo la Mama na Mtoto katika Hospitali ya Mawenzi litakamilika na kuanza kutoa huduma stahili.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**133. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE
(NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi:-

Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kuwa milipuko ya magonjwa ya Nguruwe haijitokezi mara kwa mara nchini.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

134. MHESHIMIWA PRISCUS JACOB TARIMO (MOSHI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, nini mpango wa Serikali wa kupima na kurasimisha maeneo yanayozunguka Mamlaka za Miji ili kuepuka kuendelea kuwa na makazi holela pamoja na kuweza kupeleka huduma za dharura kama Ambulance na Zimamoto.

WIZARA YA MAJI:

135. MHESHIMIWA DKT. PIUS STEPHEN CHAYA (MANYONI MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi wa maji wa Kintinku – Lisilile ili Wananchi wa Vijiji 11 vya Kata ya Chikuyu, Makutupora, Maweni na Kintinku waanze kupata maji safi na salama.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

136. MHESHIMIWA DKT. DAVID MATHAYO DAVID (SAME MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:- Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi huchangia Pato la Taifa kutokana na shughuli za Utalii:-

Je, Serikali haioni kuwa umefika wakati wa kuukarabati Uwanja wa Ndege wa Same Mjini ili ndege ndogo na za kati ziweze kutua kuleta Watalii wa ndani na nje ya nchi katika Hifadhi ya Mkomazi.

137. MHESHIMIWA CHARLES JOHN MWIJAGE (MULEBA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Visiwa vilivyopo katika Ziwa Victoria Wilayani Muleba havina usafiri salama na wa uhakika na vilevile bandari ndogo ya Kyamkwikwi haina miundombinu stahili:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kutekeleza ahadi ya Mhe. Rais ya kupeleka kivuko ili kurahisisha usafiri kati ya Visiwa vilivyopo Ziwa Victoria na Miji ya Mwambao ya Ziwa hilo Wilayani Muleba;

(b) Je, ni lini Serikali itajenga miundombinu muhimu ikiwemo maghala ya kuhifadhiya bidhaa katika Bandari ndogo ya Kyamkwikwi ili kuwavutia Wafanyabiashara kutumia Bandari hiyo.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

138. MHESHIMIWA JACQUELINE KAINJA ANDREW (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

- Je, ni lini Serikali italiangalia Zao la Asali na kulitafutia soko la uhakika ndani na nje ya nchi.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
23 APRILI, 2021**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**